

TANGAZO LA SERIKALI Na. 148 la tarehe 7/3/2025

SHERIA YA USIMAMIZI WA USHURU WA BIDHAA,

(SURA YA 147)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE SAMANI ZA MAHAKAMA YA TANZANIA YA MWAKA, 2025

Jina na
kuanza
kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye Samani za Mahakama ya Tanzania ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 6 Februari, 2025.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yanavyoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kwa bidhaa zilizoainishwa katika Jedwali, zilizoingizwa nchini au kununuliwa na Mahakama ya Tanzania au kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania kabla ya kutolewa kwa kibali cha forodha kwa ajili ya kutumika katika Mradi wa Citizen-Centric Judicial Modernization and Justice Delivery, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utatakiwa kulipwa kama vile Amri hii haijatolewa ikiwa orodha ya samani zilizooombewa msamaha zitatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itakoma kutumika ifikapo tarehe 5 ya mwezi Agosti mwaka 2025.

Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa Kwenye Samani Za Mahakama ya Tanzania

Tangazo la Serikali Na.148 (Linaendelea.)

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

BIDHAA

Na.	Aina ya bidhaa	Code	Idadi	Sehemu ya ununuzi wa bidhaa (Ndani ya nchi au nje ya nchi)
1.	Reception Chairs RC-1	94032090	200	Imported/locally
2.	Judge's Head Chairs	94032090	67	Imported/locally
3.	Magistrate's Head Chairs	94032090	107	Imported/locally
4.	One Seater Office Sofa (Inclusive for Judge's Cafeteria)	94016900	36	Imported/locally
5.	Two-Seater Office Sofa (Inclusive for Judge's Cafeteria)	94016900	60	Imported/locally
6.	Chief Justice's Sofas (One Seater)	94016900	10	Imported/locally
7.	Chief Justice's Sofas (Two Seaters)	94016900	8	Imported/locally
8.	Chief Justice's Head Chairs	94032090	9	Imported/locally
9.	Judge's Tea Chairs	94032090	80	Imported/locally
10.	Staff Tea Chairs	94032090	270	Imported/locally
11.	Training Chairs	94032090	688	Imported/locally
12.	Conference Chairs Inclusive of Chief Justice's Conference	94032090	295	Imported/locally
13.	Nurse Room Sofa (Reclining Sofa)	94016900	18	Imported/locally
14.	Steel Filling Cabinets	9403100	75	Imported/locally
15.	Compactors	84519000	126	Imported/locally
16.	Metal Racks	73269099	279	Imported/locally
17.	Lactation Rooms Vertical Blinders	94054090	9	Imported/locally
18.	Break Out Rooms Chairs	94032090	48	Imported/locally
19.	Engraved Court of Arms for two courtrooms	701399	64	Imported/locally
20.	Conference Chairs for Chambers	94032090	724	Imported/locally
21.	Reception Sofa	94016900	2	Imported/locally
22.	Office and Studio Chairs	94032090	15	Imported/locally
23.	Video Studio Sofa	94016900	1	Imported/locally

Dodoma,
8 Februari., 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
Waziri wa Fedha